BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 04 Oktoba, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub

Hoja ya Mjumbe kuhusu utatuzi wa changamoto kwa wakulima wa zao la Mwani.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Yanayosimamia Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria, Kurahisisha Upatikanaji wa Haki na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Waziri wa Fedha na Mipango:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar Nam. 11 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto,

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Vyama vya Ushirika Nam. 4 ya Mwaka 1986 na Kutunga Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar ya Mwaka 2018 ambayo inaweka utaratibu wa Uundaji na Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

III. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

82. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Malum za SMZ:

Katika masoko ya Mombasa na Darajani, kuna milango kadhaa ya maduka ambayo imepangishwa kwa wafanyabiashara mbali mbali.

(a) Je, milango ya maduka hiyo ni mingapi.

(b) Je, imekodishwa kwa shilingi ngapi kwa masoko yote mawili.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

52. MHESHIMIWA KHADIJA OMAR KIBANO (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

Serikali inafahamu kama kituo cha kulelea watoto Mazizini hakuna daktari ambae anaweza kuwasaidia watoto hao wanapopatwa na tatizo.

Je, ni lini daktari huyo atapelekwa katika kituo hicho cha kulelea watoto Mazizini.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

24. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alifuta ada kwa wanafunzi wa skuli za msingi, jambo ambalo lilileta hamasa kubwa kwa wazazi hasa kwenye kaya maskini na kupelekea kuongezeka kwa idadi kubwa ya wanafunzi katika skuli kwa mwaka wa masomo 2018.

(a) Je, Wizara ya Elimu imejipanga vipi kulikabili tatizo la ongezeko la wanafunzi kwenye maskuli.

(b) Je, ni wanafunzi wangapi kwa skuli zetu hasa Wilaya ya Micheweni, Kaskazini 'A', Kusini Unguja na Mkoani Pemba kwa skuli ambazo zipo karibu na madiko ya samaki, ambao walirudi kuendelea na masomo.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

4. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje): - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Wananchi wa Jozani licha ya eneo lao kuchangia sana pato la nchi kupitia utalii, lakini bado mapato hayo yanayoingia hayajawaletea manufaa kwani kwa kipindi cha miaka 15 wana changamoto kubwa ya maji safi na salama.

(a) Kitu gani kinakwamisha wananchi wa Jozani wasipelekewe huduma ya maji.

(b) Kwanini Serikali kupitia Wizara hii inachukuwa muda mrefu kufikisha huduma ya maji Jozani wakati suala hili Mwakilishi ameshalisemea muda mrefu.

(c) Je, hatua gani za haraka zitachukuliwa kuwapelekea wananchi wa Jozani huduma ya maji safi na salama.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

145. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Serikali imefanya kazi nzuri ya kuondoa tatizo la uchakavu wa barabara ya Kisauni - Shakani, mpaka Buyu kwa kuichonga kwa kiwango cha kifusi na kuleta faraja kwa wananchi.

(a) Je, ni lini barabara hiyo itawekwa lami baada ya kuanza tena kuchimbika ili iweze kuanza kurejea kama zamani.

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi wake wa Shakani - Buyu ambao walianza kupata matumaini ya barabara yao kujengwa ili kudumisha huduma zao za usafiri wa uhakika.

Wizara ya Biashara na Viwanda:

105. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada zake za kuleta maendeleo ya viwanda nchini. Zanzibar ina malighafi nyingi ikiwemo matunda mengi pamoja na vitu mbalimbali ambavyo ni bidhaa muhimu kwa ajili ya uzalishaji viwandani.

(a) Je, Serikali kwa kupitia Wizara yake ya Biashara na Viwanda, ina viwanda vingapi vinavyofanya kazi katika sekta zote.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha viwanda vikubwa na vidogo katika mwaka wa fedha wa 2018/2019.

(c) Je, Serikali imepokea maombi mangapi ya kuanzishwa kwa viwanda vya wawekezaji wa nje na ndani.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

98. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kwa muda mrefu sasa kumekuwa hakuna majibu ya uhakika kuhusu madeni ya Serikali wanayodaiwa wafanyabiashara waliokodi mashamba ya karafuu na hesabu kamili ya madeni yote.

(a) Je, madeni hayo ni kiasi gani.

(b) Je, kiasi gani yamelipwa na kiasi gani hayajalipwa.

(c) Je, wafanyabiashara gani wanaohusika na madeni hayo na hatua gani zimechukuliwa kwa waliokuwa hawajalipa mpaka sasa.

Wizara ya Afya:

16. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB ((Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Mnamo tarehe 27/3/2018, Waziri wa Afya Zanzibar alinukuliwa na vyombo vya habari akisema kuwa kuna tatizo katika kitengo cha PF3 cha Hospitali ya Mnazimmoja. Malalamiko hayo yapo muda mrefu na wananchi wanapata usumbufu hasa baada ya wagonjwa wao kupata matatizo.

(a) Je, Wizara imesharekebisha matatizo hayo.

(b) Je, utaratibu gani usio wa kirasimu utatumiwa kuhakikisha kuwa mgonjwa anapopelekwa anapatiwa matibabu kwanza na utaratibu wa PF3 ufuatie baadae endapo kama haijapatikana mapema.

(c) Je, kuna mashauriano gani yamefanyika na Jeshi la Polisi ambalo wakati mwengine wanaishiwa na fomu za PF3 na huku mgonjwa anahitaji kupatiwa matibabu ya haraka.

IV. HOJA YA MJUMBE:

Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub

Hoja ya Mjumbe kuhusu utatuzi wa changamoto kwa wakulima wa zao la Mwani.

V. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Yanayosimamia Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria, Kurahisisha Upatikanaji wa Haki na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

Waziri wa Fedha na Mipango:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar Nam. 11 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto,

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Vyama vya Ushirika Nam. 4 ya Mwaka 1986 na Kutunga Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar ya Mwaka 2018 ambayo inaweka utaratibu wa Uundaji na Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

Zanzibar,
04 Oktoba, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.